

IGP: Msipotii, tutawashurutisha

NA IRENE MARK

INSPEKTA Jenerali wa Polisi (IGP), Ernest Mangu, amewataka wananchi wasiwalazimishe askari polisi kuwashurutisha kutii sheria wakati wa uchaguzi.

Alisema jeshi lake litatoa elimu sahihi ya wajibu na haki za raia wakati wa kupiga kura na baada, huku akikiri kuwepo kwa dalili za vurugu baada ya mikutano ya kampeni zinazoendelea sasa.

IGP Mangu alisema hayo Dar es Salaam jana wakati wa mikutano wa siku mbili unaojadili amani katika kampeni, uchaguzi na nafasi ya viongozi wa dini na wanasisasa, mikutano huo umepewa jina la 'Maendeleo Dialogue'.

"Tunajua changamoto inayotukibili haşa wakati huu wa mchakato kuelekea Uchaguzi Mkuu, chama ambacho hakiamini kushindwa basi hawakujiandaa kushindana, nawasihi wagombea

wa nafasi mbalimbali kuwajengea utayari wa kupokea matokeo yoyote wafuasi wao," alisema IGP Mangu.

Profesa John Njingu wa Idara ya Sayansi ya Siasa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema hivi sasa hamasa katika siasa imeongezeka kutokana na vijana wengi waliokosa kazi kutaka mkombozi ili waepukane na ugumu wa maisha.

"Mijadala ya kisiasa hivi sasa imetawaliwa na propaganda zaidi kuliko hoja zenye mantiki... wanasiasa wanakashifiana na kuambiana lugha zisizo na staha," alisema na kueleza kuwa hiyo inaweza kuwa sababu ya kuvunjika kwa amani.

Kwa mujibu wa profesa huyo, vyombo vyahabari vimegawanyika kutokana na mahaba binafsi kwa wanasiasa, hali iliyowapata wahisani wa maendeleo, ndiyo maana mwaka

huu waangalizi 600 wa kimataifa watakuja nchini kushuhudia uchaguzi wetu.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Konrad Adenauer Stiftung (KAS) kutoka Ujerumani iliyoandaa mikutano huo, Stefan Reith, alisema kutokana na habari kubwa za magazeti hivi sasa unaweza kufikiri kuwa uchaguzi ni mapigano.

"Uchaguzi si mapigano,

tuuangalie kama mech ya mpira, mwamuzi ni Tume ya Uchaguzi... tunataka mchezo wa kuheshimiana, amani ya nchi ndiyo maendeleo ya nchi husika," alisema Reith.

Wadau mbalimbali wa maendeleo walioshiriki mikutano huo ni Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) na Baraza la Amani la Viongozi wa Dini Tanzania (IRCPT).